

## *Ich hab' noch einen Koffer in Berlin*

### *Bado ningali nina sanduku langu Berlin*

#### Muhtasari

Somo hili ni tofauti na masomo mengine. Halina sarufi wala mazoezi. Somo hili limekusudiwa kuwa zoezi la kusikiliza. Lina habari muhimu kuhusu Berlin ya siku hizi na Berlin ya zamani.

Yaliyomo katika zoezi hili la kusikiliza ni:

1. Wimbo ulioimbwa katika mwongo wa 1930, uliorikodiwa Berlin: *Peter Igelhoff, Das Spatzenkonzert*.
2. Wimbo mashuhuri *Das ist die Berliner Luft*, ulioimbwa na Lizzi Waldmüller katika mwongo wa 1930.
3. Wimbo wa kikundi *Comedian Harmonists* – kikundi mashuhuri cha nyimbo za anasa kutoka mwongo wa 1930. Nyimbo zao nyingi, kama vile *Mein kleiner grüner Kaktus*, ni mashuhuri mpaka leo. 1934 kikundi hiki kilipigwa marufuku kwa sababu waimbaji wake watatu walikuwa Wayahudi.
4. Tangazo la Redioni la mwandishi wa Kijerumani Thomas Mann (1875 – 1955), aliyehamia Uswissi 1933. 1939 alihamia Marekani na kuchukua uraiya wa Kimarekani 1944. Hutuba ya Thomas Mann ilitangazwa Mei 10, 1945, siku mbili baada ya kusalimu amri Ujerumani. Mwishoni mwa hutuba yake Thomas Mann alisema:

Thomas Mann:  
Deutsche Hörer!

(...) Ich sage: Es ist trotz allem eine große Stunde, die Rückkehr Deutschlands zur Menschlichkeit. Sie ist hart und traurig, weil Deutschland sie nicht aus eigener Kraft herbeiführen konnte. Furchtbarer, schwer zu tilgender Schaden ist dem deutschen Namen zugefügt worden, und die Macht ist verspielt. Aber Macht ist nicht alles, sie ist nicht einmal die Hauptsache, und nie war deutsche Würde eine bloße Sache der Macht. Deutsch war es einmal und mag es wieder werden, der Macht Achtung, Bewunderung abzugewinnen durch den menschlichen Beitrag, den freien Geist.

5. Vita Vikuu vya Pili vilipomalizika 1945, Ujerumani iligawanywa katika nchi mbili – Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani (Ujerumani ya Magharibi) na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Ujerumani (Ujerumani ya Mashariki). Nalo jiji la Berlin liligawanywa sehemu mbili. 1961 ulijengwa Ukuta wa Berlin. Tarehe 24 Oktoba, 1950, Jenerali wa Kimarekani Clay aliwatunukia raiya wa Berlin zawadi ya Kengele ya Amani iliyotundikwa katika Ukumbi wa Jiji wa Schöneberg na kupigwa kila siku wakati wa mchana. Machi 26, 1963, Rais John F. Kennedy aliizuru Berlin na kutoa hotuba yake mashuhuri katika ukumbi wa jiji wa Schöneberg ambako alitamka maneno yake yasiyosahaulika:

John F. Kennedy: Ich bin ein Berliner.

6. Mazungumzo yafuatayo yanaonyesha namna watu wa Berlin walivyo mabingwa wa kufanya mzaha wanapozungumza kwa lafudhi ya Berlin.

Berlinerin: Kannst du mal einkaufen gehen?  
 Berliner: Was soll ich?  
 Berlinerin: Einkaufen.  
 Berliner: Ich? Wieso denn das?  
 Berlinerin: Wieso denn nicht?  
 Berliner: Ich habe keine Lust.  
 Berlinerin: Ich auch nicht.  
 Berliner: Hör auf, ich glaube, das reicht nun, was?

7. Berlin daima lilikuwa jiji lenye watu wa tamaduni mbali mbali, wanakoishi wageni wengi. Mpaka ulipovunjwa Ukuta wa Berlin, wengi wa wakaazi wake wa kigeni walitoka Uturuki. Ifuatayo ni tafsiri ya mazungumzo ya Kituruki utakayosikia katika matangazo.

Türkin: Guten Tag.  
 Türke: Guten Tag. Was möchten Sie?  
 Türkin: Einen \*Döner.  
 Türke: Bitte – hier.

\* Döner: *Namna ya mshikaki – kipande cha nyama ya kondoo ya kuchoma iliyotiwa katika kipande cha mkate.*

8. Mwimbaji wa Kijerumani, akiwa pia mwigizaji wa sinema, Bibi Marlene Dietrich, alipata umashuhuri wake katika filamu *Der Blaue Engel (The Blue Angel)* iliyofanywa 1930. 1936 alihama Ujerumani kwenda kuishi Marekani. 1941, mara tu baada ya Marekani kuingia katika Vita Vikuu vya Pili, alivaa mavazi ya jeshi la Kimarekani na kuwatumbuiza askari jeshi wa Kimarekani waliowekwa Ulaya, kwa nyimbo zake. Mpaka alipofariki 1992, alikuwa akiishi Paris. Baada ya mwungano wa Ujerumani, alitoa ombi kuwa angependa kuzikwa Berlin. Wimbo wake *Ich hab' noch einen Koffer in Berlin* ulirikodiwa 1948. Yafuatayo ni maneno ya wimbo ulioimbwa na Marlene Dietrich.